JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

**HOTUBA YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, BW. JUMA MKOMI, KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA NNE (04) CHA SERIKALI MTANDAO FEBRUARI 06, 2024 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

---

***Mhe. George Simbachawene (Mb);*** *Waziri wa Nchi, Ofisi yaRais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

***Mhe. Dadi Horace Kolimba****; Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,*

***Dkt. Jasmine Tiisekwa;*** *Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Mha. Benedict Ndomba;*** *Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Bw. Yusuf Hamad Rashid;*** *Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

***Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,***

***Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali,***

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao,***

***Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

Kwanza kabisa, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uzima, afya njema, na kutupa fursa ya kukutana hapa leo. Ni jambo adhimu sana kwani wapo wengi waliotamani tuwe nao pamoja katika kikao kazi hiki, lakini Mungu hajawawezesha kutokana na sababu mbalimbali.

**Mhe. Waziri; -** Kwa umuhimu wa kipekee, napenda kukushukuru kwa kutenga muda na kuja hapa kushirikiana nasi katika Kikao Kazi hiki cha Nne (4) cha Serikali Mtandao, kilichoandaliwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Licha ya kuwa wewe ni Muhusika Mkuu wa Kikao Kazi hiki, kwa niaba ya watendaji wenzangu tunasema "karibu sana" na tunafarijika kuwa nawe hapa leo.

Aidha, napenda kuwashukuru viongozi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma na binafsi, Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, na Waandishi wa Habari, kwa kukubali na kutenga muda wenu kuja hapa kushiriki katika Kikao Kazi hiki.

***Mhe. Waziri;*** Hiki ni Kikao Kazi cha Nne (4) cha Serikali Mtandao, ambacho kinalenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao kutoka katika Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma, ili kupata taarifa na kujadiliana kwa pamoja kuhusu hali ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Vikao vya aina hii vimekuwa na manufaa makubwa katika jitihada za kukuza Serikali Mtandao katika taasisi za umma. uwepo wa vikao kazi hivi, umesaidia kujenga na kukuza uelewa wa pamoja, kwa wadau wote muhimu wa Serikali Mtandao, kuhusu jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao, changamoto zake, uwepo wa mikakati madhubuti ya kukabiliana na changamoto hizo na hatimaye kuimarisha Serikali Mtandaosiku hadi siku kupitia mawazo mbalimbali yanayotolewa na washiriki katika vikao hivi.

***Mhe. Waziri;*** Kupitia Vikao Kazi hivi, Mamlaka ya Serikali Mtandao chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imekuwa ikitoa taarifa ya utekelezaji wa maazimio mbalimbali yanayotokana na mawazo au ushauri unaotolewa na washiriki wa vikao hivi, ambayo kwa kiasi kikubwa yamechangia kuendelea kukua na kuimarika kwa Serikali Mtandao hapa nchini.

**Mhe. Waziri;** Katika kikao kazi cha tatu (3) cha Serikali Mtandao, kilichofanyika Februari 8 mwaka jana, jumla ya maazimio 12 yaliafikiwa, ambapo Mamlaka ya Serikali Mtandao ilipewa jukumu la kusimamia utekelezaji wake. Kama alivyoeleza Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mha. Benedict Ndomba, kuwa e-GA imetekeleza maazimio yote 12 na washiriki watasomewa taarifa ya utekelezaji wakati wa uwasilishaji wa mada mbalimbali.

***Mhe. Waziri;*** Katika kipindi cha utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imeendelea kuweka mazingira wezeshi yanayosaidia Taasisi za

Umma kutumia TEHAMA, katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na utoaji wa huduma bora kwa umma. Miongoni mwa hayo ni ujenzi na uboreshaji wa mifumo ya kitaasisi, shirikishi na ya kisekta, ambayo imesaidia si tu kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wa taasisi, bali pia utoaji bora wa huduma kwa umma.

**Mhe. Waziri;** Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, yanatokana ari na utashi wa Viongozi na Watendaji katika taasisi za umma pamoja na wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao. Kwa upande wa Serikali, tumeendelea kuweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na kiusimamizi, ili kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yaliyo sahihi na salama yanazingatiwaSerikalini.

**Mhe. Waziri;** Nitumie fursa hii kuwakumbusha wadau wote tuliokusanyika hapa leo kuwa, hatuna budi kumpongeza Jemedari wetu **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan,** kwa jitihada zake za kuhakikisha Serikali inawekeza kwenye TEHAMA. Ni jambo la kujivunia kuona **Mhe. Rais** akisisitiza matumizi ya TEHAMA Serikalini, ikiwemo kuelekeza mifumo ya TEHAMA kusomana na kubadilishana taarifa. Hii inatupa nguvu sisi kwa maana ya Wizara inayosimamia jukumu hili, kuongeza kasi ya kusimamia utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Aidha, katika kuhakikisha TEHAMA inaimarika Serikalini, Wizara itaendelea kuboresha miundo ya kiutumishi pamoja na stahiki kwa wataalamu wa TEHAMA ili kuhakikisha wanatumia taaluma zao ipasavyo kuleta matokeo chanya kwa taifa letu. Wizara inatambua kuwa, mafanikio ya Serikali Mtandao ni jumuishi kwa kada zote, nikuhakikishie kuwa Wizara itaendelea kusimamia na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kada zote ili kufanikisha ujenzi wa Serikali ya Kidijitali.

**Mhe. Waziri;** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya utumishi wa Umma na Utawala Bora imejipanga kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma, pamoja na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma mtandao kwa umma. Sanjari na hilo sisi watendaji tumedhamiria kuunga mkono juhudi za Serikali za kuleta mageuzi katika utoaji wa huduma za Serikali kidijiti.

***Mhe. Waziri***, Mageuzi katika utoaji huduma za Serikali kidijiti yanatekelezwa na wataalam wa TEHAMA waliopo Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Umma pamoja na wadau wengine TEHAMA. Hivyo basi, nitumie fursa hii kukuhakikishia kuwa, sisi wasaidizi wako tuko tayari kuendelea kuchapa kazi kwa bidii na kufanya ubunifu mkubwa ili kufikia dhamira ya **Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** ya kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kidijitali, **Mhe. Waziri;** Kwa hakika

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaridhishwa na utendaji kazi wa e-GA, kwani, imeweza kufanya mageuzi ya TEHAMA Serikalini, na kuboresha utendaji kazi wa kila siku katika taasisi za umma, kuboresha utoaji wa huduma kwa umma na kuzifanya zipatikane kuwa rahisi, haraka na kwa gharama nafuu.

**Mhe. Waziri;** Nachelea kusema mengi kwani jukumu langu si kutoa hotuba, bali ni kuongea maneno machache ili kukukaribisha wewe kuja kuzungumza na hadhira hii, ukiwa Mwenyeji wa ugeni huu ulio mbele yako. Hivyo basi, nihitimishe kwa kukushukuru tena wewe pamoja na Washiriki wote waliohudhuria Kikao Kazi hiki cha Nne cha Serikali Mtandao*. **Karibuni sana***.**

**Mhe. Waziri;** Sasa naomba nikukaribishe rasmi **Mhe. George B. Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,** ili uzungumze na hadhara hii, na hatimaye kufungua Kikao Kazi Cha Nne cha Serikali Mtadao.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza***